

## **Je, Kiswahili Nchini Uganda Ni Lugha Ya Kigeniau Lugha Ya Pili?**

Masereka Levi Kahaika

kahaika8@gmail.com

Mwanafunzi wa PhD Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Ikisiri**

*Lugha ya pili ni lugha rasmi au yenye kuhitajika kutumiwa katika masuala ya elimu, ajira na malengo mengine kama biashara, utalii na utambulisho (Saville-Troke, 2006). Lugha ya kigeni ni lugha inayofundishwa darasani bila kutumiwa katika jamii ambako inafundishwa (Aleidine, 2015). Nchini Uganda, shirika la uandaaji wa mitala la “National Curriculum Development Center (NCDC)” linapotoa orodha ya lughazinaazofundishwa katika shule za sekondari, lugha ya Kiswahili na Kiingereza huwekwa kwenye kundi ambalo halibainishiikiwa ni lugha ya pili au za kigeni. Kiarabu, Kifaransa, Kijerumanina Kilatini huwekwa kwenye kundi la lugha za kigeni. Kiganda, Kinailotikina Kinyakitarani miongoni mwa lugha za kikabila nchini Uganda zinazofundishwa na huwekwa kwenye orodha ya masomo. Makala haya yalinuia kubaini hadhi ya Kiswahili nchini Uganda ili kuwasaidia walimu kubaini mbinu mwafaka za kutumia katika kukifundisha kwa sababu mbinu za kufundisha lugha ya pili na lugha ya kigeni zinatofautiana. Pili, makala haya yaliibua swalinakulijibu katika makala hayahaya ambalo ni je, Kiswahili nchini Uganda ni lugha ya kigeni au lugha ya pili? Kwa kulijibu swali hili, imebainika kwamba, Kiswahili katika maeneo mengi nchini Uganda ni lugha ya kigeni katika maeneo machache mno ni lugha ya pili, ila walimu wengi wanaichukulia kama lugha ya pili na kuifundisha kwa kutumia mbinu za kufundisha lugha ya pili.*